# MUONGOZO WA MATUMIZI YA CHAKULA CHA KUKU



FALCON ANIMAL FEEDS LTD



# YALIYOMO


01 | Bidhaa na huduma zitolewazo na Falcon Animal Feeds Ltd

Nani anaweza kutumia bidhaa na huduma za Falcon animal feeds ltd | 14

15 | Jinsi ya kuwa wakala wa kuuza bidhaa za falcon animal feeds ltd

01

## BIDHAA NA HUDUMA ZITOLEWAZO NA FALCON ANIMAL FEEDS LTD




**CHAKULA CHA KUKU KWA DARAJA ZOTE**



**VIFARANGA**



**USHAURI WA KITAALAMU**

# 1. STARTER CRUMBLE

## CHAKULA CHA VIFARANGA

Ni chakula cha chenga chenga ambacho hutumika kwa vifaranga wa kuku wa nyama (Broiler), mayai (Layers), Chotara (nyama) na Chotara (Mayai).
Aina ya kuku na umri wake katika matumizi sahihi ya chakula hiki;

| AINA YA KUKU | UMRI (SIKU) |
|---|---|
| 1. Kuku wa nyama (Broiler) | 1-11 |
| 2. Kuku wa mayai (Layers) | 1-21 |
| 3. Kuku wa nyama (Chotara) | 1-28 |
| 4. Kuku wa mayai (Chotara) | 0-21 |




## UMUHIMU WA KUTUMIA CHAKULA HIKI.

**1. UKUAJI MZURI WA KUKU**
Starter Crumble ina virutubisho vyote muhimu na toshelezi kumfanya kifaranga kua na ukuaji mzuri.
Kuku wa nyama (Broiler) wanafikia uzito kati ya gramu 362- 414 ndani ya siku 11

**2. AFYA YA KUKU**
Starter Crumble kutoka Falcon Animal Feeds ina coccidiostat yenye uwezo mkubwa wa kuwa Kinga kuku wako dhidi ya ugonjwa wa kuhara damu (Coccidiosis).

## MATUMIZI SAHIHI YA STARTER CRUMBLE KWA VIFARANGA:

- Tumia mfuko mmoja (50kgs) kwa kuku 100
- Tumia mifuko miwili (100kgs) kwa kuku 200 na kuendelea.
- Zingatia kiasi hiki unapotumia starter na kwa idadi ya kuku wako, mfano kwa vifaranga 100 wakimaliza mfuko mmoja (50kgs) badilisha na uanze kutumia Grower Crumble.



# 2. GROWER PELLET

## CHAKULA KWA AJILI YA KUKU WA NYAMA (BROILER)

Chakula hiki kimetengenezwa kwa mfumo wa tambi chenga au punje kuwezesha ulaji mzuri wa kuku. Aina ya kuku na umri wake katika matumizi sahihi ya chakula hiki:

| AINA YA KUKU | UMRI (SIKU) |
|---|---|
| 1. Kuku wa nyama (Broiler) | 12-17 |
| 2. Kuku wa nyama (Chotara) | 29-60 |




## MATUMIZI SAHIHI YA GROWER CRUMBLE KWA VIFARANGA:

- Kwa kuku wa nyama (Broiler)
- Tumia mfuko mmoja (50kgs) kwa kuku 100
- Kwa hiyo ongeza kiasi cha mfuko mmoja (50kgs) kwa kila ongezeko la kuku 100, Mfano ukiwa na kuku 600 utatumia mifuko sita 6.

# 3. FINISHER PELLET

## CHAKULA KWA AJILI YA KUKU WA NYAMA (BROILER)

Chakula hiki kimetengenezwa kwa mfumo wa tambi. Aina ya kuku na umri wake katika matumizi sahihi ya chakula hiki;

| AINA YA KUKU | UMRI (SIKU) |
|---|---|
| 1. Kuku wa nyama (Broiler) | 18-26 |
| 2. Kuku wa nyama (Chotara) | 61-KUWAUZA |

## MATUMIZI SAHIHI YA FINISHER PELLET KWA VIFARANGA:

- Kwa kuku wa nyama (Broiler).
- Tumia mifuko miwili (100kgs) kwa kuku 100.
- Kwa hiyo ongeza kiasi cha mifuko miwili (100kgs) kwa kila ongezeko la kuku 100, Mfano ukiwa na kuku 500 utatumia mifuko kumi (10) kuwalisha.




## UMUHIMU WA KUTUMIA CHAKULA HIKI.

### UKUAJI

Chakula hiki kimetengenezwa ili kuboresha afya ya kuku hasa mmeng'enyo wa chakula (Gastrointestrial tract health)

Pia chakula hiki kina prebiotics na probiotics kwa ajili ya kuimarisha afya ya mfumo wa mmeng'enyo wa chakula

# 4. POST FINISHER

## CHAKULA KWA AJILI YA KUKU WA NYAMA (BROILER).

Chakula hiki kitumike kuanzia siku 27- 42




### UMUHIMU WA KUTUMIA CHAKULA HIKI.

**UKUAJI**

- Kina gharama ya chini
- Katika ulishaji wa chakula hiki kuku atafikia uzito wa kilo 3.2
- Pia chakula hiki kitaendelea kufanya kuku wako kuwa na afya njema katika kipindi chote.

# 5. SUPER STARTER

## CHAKULA CHA VIFARANGA

- Chakula hiki kimetengenezwa katika hali ya mashi.
- Chakula kwa ajili ya vifaranga.

Aina ya kuku na umri wake katika matumizi sahihi ya chakula hiki;

| AINA YA KUKU | UMRI (SIKU) |
| --- | --- |
| 1. Kuku wa mayai (Layers) | 0-21 |
| 2. Kuku wa nyama (Chotara) | 0-28 |
| 3. Kuku wa mayai (Chotara) | 0-21 |

### SIFA ZA CHAKULA

**1. UKUAJI WA KUKU**
Kina virutubisho vyote muhimu vinavyopelekea ukuaji mzuri wa kuku.

**2. COCCIDIOSTATS**
Chakula hiki kimewekwa coccidiostat yenye uwezo mkubwa wa kuwakinga kuku dhidi ya vimelea (Ptotozoa) vinavyo sababisha kuku kuhara damu (coccidiosis).



# 6. CHICK CRUMBLE

## 1. CHICK CRUMBLE

- Chakula hiki ni kizuri zaidi kutumika kwa vifaranga wa kuku wa mayai kwani hali ya punje huwezesha kuku kula vizuri na kupata virutubisho vyote muhimu kwa urahisi.
- Hupunguza upoteaji wa chakula kwa kumwagika




| AINA YA KUKU | UMRI (WIKI) |
|---|---|
| 1. Kuku wa Mayai (Layers) | 1-10 |
| 2. Kuku wa Mayai (Chotara) | 1-10 |



### UMUHIMU WA KUTUMIA CHAKULA HIKI.

- Kina matokeo mazuri katika ukuaji wa kuku.
- Kwa kipindi chote ambacho kuku wanatumia chakula cha chick crumble/ chick starter wanategemewa kufikia uzito wa gramu 900.
- Chakula hiki husaidia kuwakinga kuku wako na ugonjwa wa kuhara damu (Coccdiosis) kwani kimewekwa Coccidiostar yenye nguvu

# 7. DEVELOPER CRUMBLE NA GROWER MASH

## 1. DEVELOPER CRUMBLE

- Chakula hiki cha kuku wa mayai kimetengenezwa katika hali ya punje ndogo ndogo.
- Chakula hiki kinafaa zaidi kutumika kwani kuku hupata virutubisho vyote kwa urahisi.
- Pia huzuia upotezaji wa chakula pindi kuku wanapo kula.
- Hupelekea ukuaji mzuri wa kuku.

| AINA YA KUKU | UMRI (WIKI) |
|---|---|
| 1. Kuku wa Mayai (Layers) | 11-(yai la kwanza) |
| 2. Kuku wa Mayai (Chotara) | 11-(yai la kwanza) |

## 2. GROWER MASH

- Chakula hiki cha kuku wa mayai kimetengenezwa kwa hali ya Mashi matumizi ya vyakula hivi
- Vyakula hivi vitumike kwa kuku wa mayai (Layers na Chotara)




### UMUHIMU WA KUTUMIA CHAKULA HIKI.

- Katika kipindi cha matumizi ya chakula hiki kuku watafikia uzito kati ya gram 1,540 na 1,600.
- Badilisha matumizi ya chakula hiki na kuanza kutumia Layers mash baada tu ya kuona yai la kwanza bandani.
- Vyakula hivi havina Coccidiostat.

# 8. LAYERS MASH

- Chakula bora cha kuku wa mayai wanataga (Layers).
- Chakula hiki ni bora na kinatengenezwa kwa hali ya mashi

## MATUMIZI SAHIHI YA CHAKULA HIKI;

Chakula hiki kitumike kwa kuku kuanzia kipindi umeokota yai la kwanza bandani hadi wiki ya 60 au 65.

## UNAPOTUMIA CHAKULA HIKI UTAPATA YAFUATAYO:

- Utagaji mzuri wa kuku
- Mayai yenye uzito wastani na ukubwa wa wastani
- Mayai yenye kiini cha njano
- Ganda gumu la yai




## ZINGATIA

- Hakikisha unawatilia chakula toshelezi kulingana na idadi ya kuku Kwa kila mmoja anatakiwa apewe kati ya gram 120- 125 kwa siku.
- Usichanganye chakula hiki na palaza au pumba yoyote ya nafaka kwani utapunguza ubora wa chakula hiki.

# 9. CHOTARA LAYERS

- Chakula hiki kimetengenezwa maalumu kwa kuku chotara na pia kinatumika kwa kuku wa mayai (Layers)
- Chakula hiki kimetengenezwa kwa hali ya mashi

## MATUMIZI SAHIHI YA CHAKULA HIKI;

### Kuku chotara

Chakula hiki kitumike kuanzia mwanzo wa utagaji hadi pindi wamemaliza kutaga.

### Kuku wa mayai (Layers)

- Kwa kuku wa mayai chakula hiki kitumike kuku wanapofikia umri mkubwa na punguza utagaji yaani kuanzia wiki ya 65 na kuendelea hadi kuwa uza au kuanzia 75% kuja chini.
- Mayai yenye kiini cha njano





## VIFARANGA (HAPPY CHICK)

Falcon Animal Feeds Ltd pia inazilisha vifaranga wa Happy Chick wenye afya ya kutosha kuweza kuhimili hali zote za hewa, vichangamfu na vyenye muonekano mzuri.

## USHAURI WA KITAALAMU

Falcon Animal Feeds Ltd hutoa huduma ya ushauri wa kitaalamu kupitia madaktari wetu, wa matumizi stahiki ya chakula cha kuku bora kinachozalishwa kiwandani Falcon Animal Feeds Ltd na uleaji vifaranga ili kuleta tija katika biashara zao wateja wetu.

# 02 WANAOWEZA KUTUMIA BIDHAA NA HUDUMA ZA FALCON ANIMAL FEEDS LTD



Watu binafsi, wafanyabiashara, vikundi, makampuni wanaweza kununua bidhaa na kupata huduma za Falcon Animal Feeds Ltd; haswa.

Wajasiriamali binafsi- ambao ni watu binafsi, vikundi vinavyojishughulisha na ufugaji wa kuku.
Wajasiriamali binafsi- amabao wana dira na wanafanya biashara katika hali ya ufanisi.
Wajasiriamali binafsi- mawakala watakaoshirikiana na Falcon Animal Feeds Ltd kuwakilisha bidhaa na huduma zote zitakiwazo na ambao wana vigezo vya msingi kwa ajili ya ufanisi.

# 03 JINSI YA KUA WAKALA WA KUUZA BIDHAA ZA FALCON ANIMAL FEEDS LTD




Muombaji atapaswa kujaza fomu na kuiwasilisha ofisi za Falcon Animal FeedsLtd Makao makuu Dar es Salaam, kwa ajili ya mchakato unaofuata

Falcon Animal Feeds Ltd inasisitiza muombaji awasilishe kwanza wazo lake la biashara na nyaraka zote muhimu ofisini ili kukubalika kwake.



# Wasiliana nasi kupitia

Marketing.faf2019@gmail.com

+255 658 531 010 / +255 684 076 161

Falcon_animalfeeds_Tanzania

https://www.faf.co.tz/

Falcon_animal_feeds_ltd